# KAMATI YA BUNGE YA BAJETI

# MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO PAMOJA NA MAFUNGU YALIYO CHINI YAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23

# YALIYOMO

**1.0. UTANGULIZI ....... 4**

**2.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO PAMOJA NA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22 ...... 6**

2.1. Uchambuzi wa mafungu 7 ....... 6

2.2.1. Fungu 07 – Msajili wa Hazina ....... 8

2.2.2. Fungu 10: Tume ya Fedha ya Pamoja ....... 10

2.2.3. Fungu 13: Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu ....... 11

2.2.4. Fungu 21: Hazina ....... 12

2.2.5. Fungu 22: Deni la Serikali ....... 14

2.2.6. Fungu 23: Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ....... 16

2.2.7. Fungu 50: Wizara ya Fedha na Mipango ....... 17

**3.0. UCHAMBUZI WA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA FUNGU 45 – OFISI YA TAIFA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22 ....... 21**

3.1. Mwenendo wa Utolewaji wa Fedha kwa Fungu 45 ....... 21

3.2. Masuala ya Msingi yaliyobainika katika Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ....... 22

**4.0. UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO PAMOJA NA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23 ....... 24**

4.1. Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mafungu Saba ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 ....... 24

4.2. Maombi ya Fedha ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2022/23 ....... 24

**5.0. MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI FUNGU 45 KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23 ....... 26**

5.1. Maamuzi baada ya Mashauriano kuhusu Bajeti ya Fungu 45 ....... 27

**6.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI ....... 29**

6.1. Kuanzishwa kwa Fungu Jipya Namba 001 Deni la Serikali ....... 29

6.2. Utekelezaji wa Miradi kwa njia ya Ubia baina ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma ..... 29

6.3. Utendaji wa Kazi wa Kikosi kazi cha Mabadiliko ya Kodi " Task Force on Tax Reform" 30

6.4. Kutofautisha majukumu ya Idara za Serikali kati ya ukusanyaji wa mapato na utoaji wa Huduma ........ 30

6.5. Utekelezaji wa Blue Print kwa masuala ya kikodi ........ 31

6.6. Kuangalia uwezekano wa kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Manunuzi ya Umma 31

**7.0. HITIMISHO........ 33**

# MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO PAMOJA NA MAFUNGU YALIYO CHINI YAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23

## 1.0. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa kanuni ya 118(1) na (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020 naomba kuwasilisha utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na mafungu yaliyoko chini yake kwa mwaka wa fedha 2021/22 na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mafungu 8 yaliyoko chini ya Wizara pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2022/23. Makadirio ya mapato na Matumizi ya Ofisi ya Taifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yanawasilishwa na kamati hii kwa mujibu wa kifungu cha 9(1)(c) cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439 ambacho kinaipa mamlaka ya Kamati kuchambua, kushauri na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bunge ya Bajeti ilipitia na kuchambua taarifa za Wizara ya Fedha na Mipango zilizojumuisha mafungu 8 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa kuwa ni sharti la Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, na Mafungu hayo ni kama ifuatavyo:-

i. **Fungu 001** – Deni la Serikali
ii. **Fungu 007 –** Ofisi ya Msajili wa Hazina
iii. **Fungu 010 –** Tume ya Pamoja ya Fedha
iv. **Fungu 013 –** Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu

v. **Fungu 021 –** Hazina
vi. **Fungu 022 –** Huduma za Mfuko Mkuu
vii. **Fungu 023 –** Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali
viii. **Fungu 050 –** Wizara ya Fedha na Mipango
ix. **Fungu 045** – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Kamati imegawanyika katika maeneo makuu matatu kama ifuatavyo: -

i. Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango, Mafungu yaliyo chini yake pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2021/22;

ii. Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2022/23;

iii. Maoni na Mapendekezo ya Ujumla ya Kamati.

## 2.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO PAMOJA NA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya fedha na Mipango ina Mafungu 8 pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi fungu 45. Jedwali Na 1 linaonyesha mwenendo wa utekelezaji wa bajeti za mafungu 7 yaliyo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango

### 2.1. Uchambuzi wa mafungu 7

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya mafungu yote yaliyo 7 ya Wizara ya Fedha Mwaka wa Fedha 2021/22. Katika mwaka 2021/22, mafungu saba (7) ya Wizara ya Fedha na Mipango yaliidhinishiwa na Bunge jumla ya **Shilingi trilioni 12.95** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya kiasi hicho, **Shilingi trilioni 11.93** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi trilioni 1.03** kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Aidha, kati ya **Shilingi trilioni 11.93** za matumizi ya kawaida malipo ya Deni la Serikali yalikuwa ni **Shilingi trilioni 8.834** na shilingi **trilioni 3.096** zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida pamoja na mishahara kwa Idara, Vitengo na Taasisi zilizo chini ya Wizara na mipango. Aidha, kiasi hicho kilijumuisha michango ya mwajiri kwenye Mifuko ya Hifadhi za Jamii; na stahili za Viongozi Wakuu wa Serikali pamoja na **Shilingi bilioni 480.72** kwa ajili ya Marekebisho ya mishahara ya watumishi wa umma Majaji; na Viongozi Wakuu wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa miradi ya maendeleo zilitengwa jumla ya **Shilingi trilioni 1.24 kati ya fedha hizo** Shilingi **bilioni 992.22 ni fedha za ndani** na Shilingi **bilioni 244.11** ni fedha za nje. Jedwali na 1 hapo chini linaonyesha

utekelezaji wa Bajeti kwa mafungu 7 ya Wizara ya Fedha na Mipango bila kuhusisha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali

**Jedwali Na. 1 Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango Mafungu 8 pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi fungu 45 kwa mwaka 2021/22**

| Fungu | Bajeti iliyoidhinishwa 2021/22 | Fedha iliyotolewa hadi Aprili, 2022 | Asilimia ya Bajeti Iliyoidhinishwa |
|---|---|---|---|
| **07. Msajili wa Hazina** | | | |
| Mishahara | 3,859,834,000.00 | 3,444,170,944.04 | 89.23 |
| Matumizi mengineyo | 57,229,786,002.00 | 60,453,820,683.91 | 105.63 |
| Maendeleo Ndani | 1,000,000,000.00 | 1,000,000,000.00 | 100 |
| Maendeleo Nje | 1,300,000,000.00 | 429,170,000.00 | 33.01 |
| **Jumla Ndogo** | **63,389,620,002.00** | **65,327,161,627.95** | **103.06** |
| **10 Tume ya Pamoja ya Fedha** | | | |
| Mishahara | 716,795,000.00 | 632,324,023.70 | 88.2 |
| Matumizi mengineyo | 2,119,104,828.00 | 1,630,581,391.34 | 79.6 |
| **Jumla Ndogo** | **2,835,899,828.00** | **2,262,905,415.04** | **81.84** |
| **013 Kitengo cha udhibiti fedha haramu** | | | |
| Matumizi mengineyo | 2,915,586,000 | 2,728,374,500.85 | **93.5** |
| Maendeleo Ndani | - | 143,137,292.93 | **-** |
| Maendeleo Nje | 400,000,000 | - | **-** |
| **Jumla Ndogo** | **3,315,586,000** | **2,871,511,793.78** | **86.6** |
| **021Hazina** | | | |
| Mishahara | 419,927,650,000.00 | 175,838,201,949.97 | 41.8 |
| Matumizi mengineyo | 644,200,565,000.00 | 305,901,979,090.80 | 47.4 |
| Maendeleo Ndani | 975,013,499,000.00 | 181,593,127,142.57 | 18.6 |
| Maendeleo Nje | 234,740,000,000.00 | 241,051,506,129.21 | 102.6 |

| Fungu | Bajeti iliyoidhinishwa 2021/22 | Fedha iliyotolewa hadi Aprili, 2022 | Asilimia ya Bajeti Iliyoidhinishwa |
|---|---|---|---|
| **Jumla Ndogo** | **2,063,473,550,000.00** | **904,384,814,312.55** | **43.8** |
| **022 Huduma ya mfuko mkuu** | | | |
| Mishahara | 9,275,296,000.00 | 7,968,686,073.96 | 85.91 |
| Matumizi mengineyo | 10,664,243,143,000 | 8,752,805,801,479.54 | 82.08 |
| **Jumla Ndogo** | **10,673,518,439,000** | **8,760,774,487,553.50** | **82.08** |
| **23.Idara ya mhasibu mkuu** | | | |
| Mishahara | 5,967,732,000 | 5,070,382,975.07 | 84.9 |
| Matumizi mengineyo | 38,551,734,000 | 33,334,078,662.20 | 86.4 |
| Maendeleo Ndani | 2,000,000,000 | 2,000,000,000.00 | 100 |
| Maendeleo Nje | 1,669,650,000 | 1,122,200,000.00 | 67.2 |
| **Jumla ndogo** | **48,189,116,000** | **41,526,661,637.27** | **86.1** |
| **50.Wizara ya fedha na mipango** | | | |
| Mishahara | 40,902,869,000.00 | 35,595,272,724.40 | 87.02 |
| Matumizi mengineyo | 37,600,514,000.00 | 37,924,991,536.73 | 100.86 |
| Maendeleo Ndani | 14,208,880,000.00 | 6,805,977,391.73 | 47.89 |
| Maendeleo Nje | 6,002,386,000.00 | 3,561,145,000.00 | 59.33 |
| **Jumla Ndogo** | **98,714,649,000** | **83,887,386,652.86** | **84.98** |
| **Jumla Kuu** | **12,953,365,897,002.00** | **9,861,034,928,992.95** | **76.12** |

*Chanzo:Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa fedha 2021/22*

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa Kamati ilifanya uchambuzi wa kina wa utekelezaji wa Bajeti na masuala yaliyobainika ni kama ifuatavyo:-

### 2.2.1. Fungu 07 – Msajili wa Hazina

**Mheshimiwa Spika,** Mwaka wa Fedha 2021/22 Ofisi ya Msajili wa Hazina, iliidhinishiwa kiasi cha **Shilingi bilioni 63.39** kwa

ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 3.86** zilitengwa kwa ajili ya mishahara, **Shilingi bilioni 10.23** kwa ajili ya uendeshaji wa ofisi na **Shilingi bilioni 47**. kwa ajili ya matumizi maalumu kama vile kulipa madeni ya Mashirika na Taasisi za Umma na kurekebisha Mashirika yenye matatizo ya mitaji. Kwa upande wa fedha za maendeleo zilitengwa **Shilingi Bilioni 2.3**, kati ya hizo **Shilingi bilioni 1.0** fedha za ndani na **Shilingi Bilioni 1.3** fedha za nje. Hadi kufikia mwezi Aprili fungu hili lilipokea jumla ya **Shilingi bilioni 65.33** sawa na **asiilimia 103.06** fedha hizo zimezidi kiwango cha Bajeti kutokana na fedha za uhamisho kujumuishwa kwenye Bajeti ya Fungu husika pamoja na malipo kwenda Benki ya Exim China kuhusu kiwanda cha nguo cha Urafiki. Utekelezaji wa matumizi ni kama unavyoonekana kwenye jedwali Na 1. Kamati ina maoni yafuatayo kuhusu utekelezaji wa Bajeti wa Fungu hili:-

**a) Matumizi Maalum**

**Mheshimiwa Spika,** Matumizi maalum ni muhimu sana kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa sababu ndiyo hutumika kurekebisha mitaji kwa mashirika ya umma yenye changamoto ya mitaji pamoja na kulipa madeni ya Serikali iliyoyarithi kutoka iliyokuwa CHC-Consolidated Holding Corporation. Hadi kufika mwezi Aprili zilikuwa zimetolewa jumla ya **Shilingi bilioni 25.4** kati ya shilingi **bilioni 47.0** zilizokuwa zimetengwa sawa na **asilimia 54.14**. Kiasi hicho kilichotengwa mbali na kwamba kilikuwa kidogo ukilinganisha na mahitaji imesababisha Serikali kuendelea kutolipa madeni kikamilifu inayodaiwa na Wananchi katika maeneo mbalimbali na kuwezesha Taasisi zake kimtaji. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inawezesha Ofisi msajili wa hazina kifedha ili iweze kutoa mitaji kwa Makampuni na Taasisi za umma kama vile Benki ya Kilimo na Benki ya

Uwekezaji ili ziweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Kamati inaamini kuiwezesha ofisi hii ni kuongeza mapato ya Serikali yasiyotokana na kodi.

**b) Uhaba wa Watumishi**

**Mheshimiwa Spika,** Utofauti wa Ofisi hii na Ofisi nyingine za Umma ni kwamba Ofisi hii inasimamia uwekezaji wa mitaji ya Umma na inakusanya marejesho ya mitaji ya hiyo. Hivyo si sawa Ofisi hii kutokuwa na watumishi wa kutosha. Mathalani kati ya watumishi 185 wanaohitajika Ofisi watumishi waliopo ni 145 tu hivyo kuna upungufu wa watumishi 40. Hali hii inaathiri utendaji kazi wa Ofisi, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba Ofisi hii inapata watumishi wa kutosha ili itekeleze majukumu yake kikamilifu.

### 2.2.2. Fungu 10: Tume ya Fedha ya Pamoja

**Mheshimiwa Spika,** Tume ya Fedha ipo kwa mujibu wa Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Katika mwaka wa fedha 2021/22 Tume ilitengewa jumla ya **Shilingi bilioni 2.84** ambapo, **Shilingi bilioni 2.12** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, na **Shilingi milioni 716.7** ni kwa ajili ya Mishahara. Hadi mwezi Aprili 2022 Fungu hili lilikuwa limepokea jumla ya **Shilingi bilioni 2.26** sawa na **asilimia 81.84** ya Bajeti yake ya Mwaka wa Fedha 2021/22. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 632.32** ni mishahara na **Shilingi bilioni 1.630** ni fedha za Matumizi Mengineyo. Kamati ina maoni na ushauri ufuatao katika fungu hili.

**Mheshimiwa Spika,** Tume ya pamoja ya Fedha imekwisha fanya tafiti kwenye maeneo makuu mawili moja ni kuhusu Ukusanyaji wa Mapato ya Muungano yanayotokana na Huduma za Mawasiliano ya Simu, Fedha na Bima kwa

kampuni/mashirika yaliyosajiliwa upande mmoja wa Muungano na kufanya Biashara katika Pande zote Mbili za Muungano na uanzishwaji wa Akaunti jumuifu ya fedha. Kwakuwa, tafiti hizi zimekamilika Kamati inaishauri Serikali kuzifanyia kazi kikamilifu ili kuondoa kero za Muungano zinazojitokeza katika maeneo hayo.

### 2.2.3. Fungu 13: Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2021/22, Fungu 13 liliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi bilioni 3.88** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 3.48** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi milioni 400** ni fedha za nje kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Aidha, Wizara ilifanya uhamisho na kuliongezea fungu hili kiasi cha **Shilingi milioni 707.365** na kufanya bajeti kwa fungu hili kuwa jumla ya **Shilingi bilioni 4.023**

**Mheshimiwa Spika,** Hadi mwezi Aprili 2021 kitengo kilikuwa kimepokea Shilingi **Bilioni 2.871** sawa na **asilimia 71.38** ya Bajeti yote ya Fungu. Aidha, fungu hili halikupokea fedha yoyote ya maendeleo kutoka nje licha ya kwamba zilitengwa kiasi cha **Shilingi milioni 400** fedha za nje. Vilevile fungu hili limepokea kiasi cha **Shilingi milioni 143.14** fedha za ndani ambazo hazikuwa zimetengwa awali. Kamati ina maoni na mapendekezo yafuatayo kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya fungu hili.

#### a) Kuanzisha Mamlaka ya Kudhibiti Fedha haramu

**Mheshimiwa Spika,** ili kitengo hiki kifanye kazi yake kwa ufanisi Kamati inaishauri Serikali kitengo hiki kipewe hadhi ya kuwa Mamlaka Kamili kuliko ilivyo hivi sasa ambapo asilimia karibia 90

ya watumishi wake ni wa kuazima kutoka mafungu na Taasisi nyingine.

**b) Kuhakikisha kwamba Kitengo kinakuwa na rasilimali fedha na rasilimali watu toshelezi**

**Mheshimiwa Spika,** hadi mwezi Aprili, 2022 kitengo kilikuwa kimepokea Taarifa ya jumla ya miamala **Shuku 12,840** kati ya miamala hiyo **miamala 2,186** ilihusu usafirishaji wa fedha kutoka na kuingia nchini; **Miamala 5,251** ilihusu fedha taslimu, **Miamala ya 5,403** ilihusu kutuma fedha kwa njia ya kielektroniki. Jambo ambalo linasikitisha ni kwamba miamala ambayo uchunguzi umekamilika na kuwasilishwa taarifa zake fiche za fedha kwa vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria ni **101** tu sawa na **asilimia 0.78**. Madhara yake ni fedha za wananchi kuendelea kushikiliwa katika mabenki na Taasisi za fedha na hivyo kuleta taharuki. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba kitengo hikii kinawezehswa kifedha na rasilimali watu ili kuondoa taharuki hiyo.

### 2.2.4. Fungu 21: Hazina

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2021/22, Fungu 21 liliidhinishiwa kiasi cha **shilingi trilioni 2.06**, kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Maendeleo. Kati ya kiasi hicho, **Shilingi trilioni 1.06** zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi bilioni 999.35** zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha, matumizi ya kawaida ambayo ni **Shilingi** trilioni **1.06** yamegawanywa katika matumizi yafuatayo **Shilingi bilioni 419.93** ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Idara na Vitengo vya Hazina, **Shilingi bilioni 209.98** ilikuwa ni kwa ajili ya marekebisho ya mishahara kwa watumishi wa umma na **Shilingi bilioni 644.2** kwa ajili ya matumizi maalumu ya kitaifa na mahitaji ya dharura yanayojitokeza katika mafungu

mbalimbali wakati wa utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali. Kwa upande wa maendeleo Kati ya **Shilingi bilioni 999.345** zilizotengwa **Shilingi bilioni 975.01** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 24.33** ni fedha za nje. Aidha, Wizara ya Fedha ilifanya uhamisho wa kiasi cha **Shilingi bilioni 392.926** kwa ajili ya marekebisho ya mishahara na kupandishwa vyeo watumishi kutoka katika fungu hili na kufanya fungu hili kuwa na bajeti ya **Silingi trilioni 1.904.**

**Mheshimiwa Spika,** Hadi Aprili 2022, Fungu 21 limepokea jumla ya **Shilingi bilioni 904.39** sawa na **asilimia 47.47** ya makadirio ya **Shilingi trilioni 1.904.** Kati ya kiasi hicho, **Shilingi bilioni 175.84** ni kwa ajili ya mishahara na **Shilingi bilioni 305.902** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Kwa upande wa fedha za maendeleo zilipokelewa jumla ya **Shilingi bilioni 422.64**, kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 181.593** ndani na **Shilingi bilioni 241.051**. Jedwali namba 1 limeonyesha mwendo wa utekelezaji wa Bajeti. Pamoja na mwenendo huo uchambuzi wa kamati imebaini masuala mbalimbali na inaushauri ufuatayo:-

**a) Changamoto za Watumishi katika Taasisi ambazo ziko chini ya Wizara ya Fedha na Mipango**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini Mamlaka ya Mapato Tanzania inahitaji jumla ya **watumishi 8,374** watumishi waliopo ni **6,055,** Sawa na upungufu wa **watumishi 2,319.** Kamati inaishauri Serikali kuiangalia Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa jicho la kipekee kwa sababu hapa ndipo mapato yanapokusanywa na kutumika maeneo mengine. Aidha, Kamati inatambua juhudi ambazo Serikali imeendelea kuchukua za kuongeza watumishi sehemu ambazo inakusanya mapato, kama ilivyofanya Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kuajiri watumishi takriban 2000.

**b) Uanzishwaji wa Mfuko wa Dharura *“Contigency Fund”***

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Dharura umeanzishwa kwa mujibu wa ibara ya 140 ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano ya mwaka 1977. Aidha, ibara hiyo inatoa fursa kwa Bunge kutunga sheria ya uanzishwaji wa mfuko huo. Bunge lilitekeleza majukumu yake na likatunga Sheria ya Bajeti sura ya 439 na katika kifungu cha 35 hadi 38 kinaweka utaratibu wa vyanzo vya mapato vya mfuko na namna ya kuutumia. Hivi sasa Fedha za dharura zimekuwa zikitengwa kupitia fungu 21 na hivyo matumizi yake hayafuati sheria ya Bajeti kwa sababu si mfuko. Kamati inataka Serikali kuanzisha mara moja mfuko huo ili utusaidie tunapokuwa na dharura kama vile za ugonjwa wa UVIKO-19 na maafa pamoja na hili linalotukabili sasa la upandaji wa bei za mafuta.

**c) Kuimarisha kitengo cha ubia kati ya sekta ya umma na sekta Binafsi**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuimarisha kitengo hiki kwa kukiongezea bajeti ili kiweze kutekeleza majukumu yake kama ilivyokusudiwa pamoja na kuanzisha mfuko wa kusaidia kuandaa na kuendeleza miradi ya PPP “PPP Facilitation Fund”.

### 2.2.5. Fungu 22: Deni la Serikali

**Mheshimiwa Spika,** Fungu 022 katika mwaka wa fedha 2021/22 liliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi trilioni 10.67** Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 9.275** ni kwa ajili ya mishahara ya maafisa wa umma wanaolipwa kupitia Fungu 022, **Shilingi trilioni 4.90** ni kwa ajili ya malipo ya deni la Ndani, **Shilingi trilioni 3.931** kwa ajili ya deni la Nje na **Shilingi trilioni 1.829** ni kwa ajili Huduma za Mfuko Mkuu. Aidha, Wizara ya Fedha

ilifanya uhamisho wa kiasi cha **Shilingi bilioni 3.6** kutoka katika fungu hili na kwenda fungu 23 Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali na kufanya fungu hili kuwa na bajeti ya **Shilingi trilioni 10.669.**

**Mheshimiwa Spika,** hadi mwezi Aprili, 2022 jumla ya **Shilingi trilioni 8.76** zilitolewa ikiwa ni **asilimia 82.03** ya bajeti. Mchanganuo wa matumizi ni kama ifuatavyo; **Shilingi bilioni 7.97** ni mishahara ya maafisa wa umma wanaolipiwa Fungu kupitia fungu hili, **Shilingi trilioni 8.75** ni kwa ajili ya malipo ya Deni la Serikali pamoja na michango ya mwajiri kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii, bima ya afya, mfuko wa fidia kwa wafanyakazi na malipo ya pensheni kwa wastaafu wanaolipwa Hazina.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaushauri ufuatao kuhusiana na malipo ya Deni la serikali:-

a) **Maombi ya Kuahirisha ulipaji wa Deni "Debt Suspension"**

**Mheshimiwa Spika,** Hivi sasa Serikali yetu iko kwenye mazungumzo na nchi wanachama wa Paris (Paris Club) na wasio wanachama (Non Paris) pamoja na zile zilizotukopesha kwa njia ya *Bilateral* ili kuangalia uwezekano wa kuahirisha ulipaji wa madeni. Jambo hili lina mitazamo miwili mtazamo wa kwanza ni hatua hii inatoa ahueni kwenye Bajeti *"Fiscal space"* ya kufanya miradi mingine kutokana na ahirisho hilo. Lakini upande mwingine ambao ni lazima uangaliwe muda utakapofika wa kulipa lazima mapato yawe na uwezo wa kubeba madeni yaliyoiva wakati huo na yaliyoahirishwa. Hivyo basi, lazima Serikali ifanye tathmini ya kina na kuangalia endapo mapato yataweza kubeba mzigo huo kabla ya kuomba ahirisho. Vilevile,

Serikali itafute namna ambavyo itasaidia kuongeza mapato ya fedha za kigeni ili kufanya deni la Serikali kuendelea kuwa himilivu mfano kutumia vyanzo bunifu vya fedha kama vile infrastructure bonds, mfuko wa mazingira kupitia "carbon credit".

### 2.2.6. Fungu 23: Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali iliidhinishiwa kiasi cha **Shilingi bilioni 48.189** Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 3.67** ni fedha za Maendeleo na **Shilingi bilioni 44.519** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha, fungu hili liliongezewa kiasi cha Shilingi **bilioni 3.6** kutoka fungu 22 Deni la Serikali na kufanya fungu hili kuwa na jumla ya bajeti ya **Shilingi bilioni 51.789.** Hadi mwezi Aprili, 2022 jumla ya **Shilingi bilioni 41.526** zimetolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo sawa na **asilimia 86.1** ya Bajeti ya Mwaka. Kati ya kiasi hicho, **Shilingi bilioni 5.07** ni kwa ajili ya mishahara, **Shilingi bilioni 33.334** ni matumizi ya kawaida na **Shilingi bilioni 3.122** ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Mchanganuo wa utekelezaji wa bajeti kwa fungu hili ni kama unavyoonekana katika jedwali na 1.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na kwamba fungu hili lina ofisi Mikoa yote Tanzania bara lakini ndilo fungu ambalo lina Bajeti ndogo ukilinganisha na majukumu yake. Fungu hili lina majukumu makubwa yafuatayo:- usimamizi wa Sheria ya Fedha za umma SURA 348; Kuandaa Miongozo ya Uhasibu (Accounting Manual), Nyaraka za Uhasibu (Accounting Circulars) na Nyaraka za Hazina (Treasury Circulars), kutathmini utekelezaji wake katika kuhasibu mapato, matumizi na mali za Serikali na kuratibu maboresho ya Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348 na Kanuni zake; Kushauri na kutoa ufafanuzi kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) na

Kamati ya kudumu ya Bunge ya Serikali za Mitaa (LAAC) kuhusiana na masuala ya usimamizi wa Fedha za Umma pamoja na kulipa kiinua mgongo na pensheni kwa wastaafu wanaolipwa kupitia Hazina.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kutimiza azma hiyo baada ya majadiliano baina ya Kamati na Serikali, ilibainika kwamba fungu hili lina mahitaji makubwa ya kufanya mafunzo kwa Halmashauri zote nchini kuhusiana Na Mifumo mbalimbali ya kiuhasibu. Hivyo, Kamati iliiagiza Wizara ya Fedha na Mipango kupunguza kiasi cha **Shilingi bilioni 1** kutoka kwenye vifungu vya Fungu 21 ili ziende kuwezesha utolewaji wa mafunzo na utekelezaji wa majukumu ya fungu hili. Wizara ilikubali na fedha hizo zilihamishwa kutoka fungu 21 kwenda fungu 23.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa mifumo mingi ya Serikali imekuwa ikijengwa na vijana wa Kitanzania ni jambo la kupongeza, hata hivyo Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuendelea kuwekeza kwenye mifumo na kuhakikisha mifumo hiyo inasomana.

### 2.2.7. Fungu 50: Wizara ya Fedha na Mipango

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2021/22, fungu 50 liliidhinishiwa jumla ya **Shilingi bilioni 98.714** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 78.503** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa Idara na taasisi zilizo chini ya Fungu 50 na **Shilingi bilioni 20.211** ni kwa ajili ya mradi ya maendeleo. Aidha, Wizara ilifanya uhamisho wa fedha na kuliongezea fungu hili kiasi cha **Shilingi bilioni 10.333** na kulifanya fungu hili kuwa na bajeti ya **Shilingi bilioni 109.048.**

**Mheshimiwa Spika,** Hadi mwezi Aprili 2022 fedha zilizokuwa zimepokelwa ni **Shilingi bilioni 83.887** sawa **asilimia 76.93** ya makadiro ya mwaka 2021/22. Kati ya kiasi kilichopokelewa **Shilingi bilioni 35.59** ni kwa ajili ya mishahara, **Shilingi bilioni 37.924** ni fedha za matumizi mengineyo na **Shilingi bilioni 3.562** fedha za nje na **Shilingi bilioni 6.806** fedha za ndani za maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi wa utekelezaji wa Bajeti ya fungu hili kwa kulinganisha na majukumu ya Fungu hili na ina maoni na mapendekezo yafuatayo:-

**a) Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali**

**Mheshimiwa Spika**, kuna haja ya kufanya mabadiliko ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma ili kuleta tija kwenye kitengo cha ukaguzi wa ndani. Changamoto zinazosababishwa na sheria ilivyo hivi sasa ni kama ifuatavyo:-

i. Kitengo cha ukaguzi wa ndani kinawasilisha Taarifa yake kwenye Kamati ya ukaguzi ambayo ina wajumbe 5, watatu kutoka Taasisi husika na wawili kutoka nje ambao wote wanateuliwa afisa masuuli wa fungu husika. Taratibu za kimataifa zinahitaji walau watatu watoke nje ya fungu au Taasisi husika;

ii. Kitengo cha ukaguzi wa ndani kiko chini ya Afisa masuuli na kinapata Bajeti chini ya fungu husika hivyo inaondoa uhuru wa ukaguzi;

iii. Kitengo kushindwa kufanya ukaguzi stahiki kutokana na kuwa mifumo hafifu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapendekeza kwamba kwanza kufanya marekebisho kwenye sheria ya ukaguzi ili wakaguzi wa ndani wawajibike kwa mkaguzi Mkuu wa ndani na Kamati ya

ukaguzi wajumbe wabadilishwe watatu watoke nje na wawili watoke ndani. Na endapo itatokea kwamba kamati haijakubalina na majibu ya manejimenti mkaguzi wa ndani aruhusiwe kuwasilisha Taarifa yake kwa Mkaguzi Mkuu wa Ndani moja kwa moja kwa hatua zaidi. Aidha, inashauriwa kwamba Idara ya Mkaguzi Mkuu wa ndani iwe na fungu lake peke yake ili iwe na uhuru wa kukagua na kutoa maoni.

**b) Idara ya Usimamizi wa Mali za Serikali**

**Mheshimiwa Spika,** Kuna changamoto kubwa katika uuzaji wa mali za Serikali ambazo ama zimechakaa au Serikali inahitaji kuziuza kwa sababu mbalimbali. Ofisi za Umma maeneo mengi nchini zina mali za umma ambazo hazitumiki lakini imekuwa vigumu ama kuziuza au kuziharibu. Matokeo yake Ofisi za Umma zimekuwa kama maeneo ya maegesho ya magari machakavu, samani na vifaa vya tehama. Changamoto hii ni kubwa zaidi kwa balozi zetu ambapo haziwezi ama kuharibu au kuuza mali ambazo hazitumiki mpaka wataalam kutoka idara hii watakapothibitisha. Jambo la kushangaza ni pale ambapo wakati mwingine gharama inayotumika kuhakiki mali hizo chakavu ni kubwa kuliko thamani ya mali zinazohakikiwa. Hivyo kuna haja ya Serikali kupitia upya Sheria na utaratibu wake wa kuuza na kuharibu mali chakavu ili ufanyike kwa ufanisi na kwa gharama ndogo.

**c) Idara ya Usimamizi wa Mifumo ya Serikali**

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na kwamba Serikali inaendelea kuhuisha mifumo yake ili kuondoa changamoto za kupanga na kutumia fedha za umma. Bado kwa kiasi kikubwa mifumo hii haijawa na ufanisi uliotarajiwa kutokana na kutofungamanishwa na mifumo mingine na kukosekana kwa mtandao wa uhakika.

Kamati inatambua juhudi za Serikali katika kufungamanisha mifumo hii hata hivyo suala hili limekuwa linatekelezwa polepole. Hivyo, ni vyema Serikali ikaongeza kasi katika katika kuhuisha mifumo yake ili isomane na ifanye kazi kwa ufanisi.

## 3.0. UCHAMBUZI WA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA FUNGU 45 – OFISI YA TAIFA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22

**Mheshimiwa Spika,** Jukumu la kujadili kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Taifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo linatekelezwa na Kamati ya Bajeti kwa mujibu wa Kifungu cha 9(1) kipengele (c) cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439. Katika kutekeleza jukumu hilo Kamati ya Bajeti ilikutana na Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Mdhibiti na Kaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kufanya mashauriano kuhusu utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu hili.

### 3.1. Mwenendo wa Utolewaji wa Fedha kwa Fungu 45

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 ilitengewa Jumla ya **Shilingi bilioni 80.09** kati ya Fedha hizo **Shilingi bilioni 13.35** ni kwa ajili ya mishahara na **Shilingi bilioni 54.84** zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, **Shilingi bilioni 11.91** zilikuwa ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo**.** Hadi mwezi Aprili Fungu hilo lilikuwa limepokea jumla ya **Shilingi bilioni 61.03** sawa na **asilimia 76.19** ya Bajeti mchanganuo wa utolewaji wa fedha ni kama unavyoonekana kwenye jedwali Na 2 Hapo chini.

**Jedwali Na 2. Mchanganuo wa Fedha za Matumizi zilizotolewa hadi Aprili 2022**

| Aina ya Matumizi | Bajeti iliyoidhinishwa 2021/22 | Fedha iliyotolewa hadi Aprili 2022 | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Mishahara | 13,346,294,000 | 12,017,153,517 | 90.04 |
| Matumizi Mengineyo | 54,838,739,000 | 45,847,492,216 | 83.60 |
| Maendeleo Ndani | 9,200,000,000 | 2,854,735,166 | 31.03 |
| Maendeleo Nje | 2,714,902,000 | 309,745,000 | 11.4 |
| JUMLA | 80,099,935,000 | 61,029,125,899 | **76.19** |

*Chanzo: Randama Fungu 45*

## 3.2. Masuala ya Msingi yaliyobainika katika Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali

**Mheshimiwa Spika,** Katika majadiliano masuala yafuatyo yalibainika ambayo kamati iliyatolea maelekezo kwa Serikali:-

i. Ofisi ya mdibiti na mkaguzi mkuu wa Serikali ina changamoto ya watumishi na hivyo kuathiri utendaji kazi wake;

ii. Ujenzi wa Ofisi za CAG mikoani ili kuwaondoa wakaguzi wa Ofisi ya Mdhibiti Mkuu na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutoka kwenye majengo ya wakaguliwa unaendelea kwa kusua sua kutokana na utengaji na utolewaji hafifu wa fedha;

iii. Bado Ofisi ya CAG haina uhuru wa kuajili wataalamu wenye ujuzi na utaalamu unaotakiwa katika Ofisi hiyo na badala yake ajira bado zinaamuliwa na Tume ya Ajira;

iv. Majukumu ya ukaguzi yanaongezeka kwa kasi kuliko ongezeko la rasilimali fedha; na

v. Upungufu Mkubwa wa magari kwa ajili ya kaguzi mbalimbali kama vile za Ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na changamoto hizo kamati ilishauri Serikali kwanza kuhakikisha inatoa fedha zote za maendeleo zilizosalia kwa fungu hili; Inahakikisha walau kila mwaka Ofisi inaajili watumishi wapya ili kuondoa changamoto ya watumishi na Serikali iwe na jukumu la kutoa kibali tu lakini nani anaajiliwa na kwa taaluma zipi jukumu hili liachiwe Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yenyewe.

## 4.0. UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO PAMOJA NA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23

### 4.1. Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mafungu Saba ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2022/23

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2022/23, Wizara ya Fedha na Mipango inaomba kuidhinishiwa matumizi ya jumla ya **Shilingi trilioni 14.94** kwa mafungu yote nane (8). Kati ya kiasi hicho, **Shilingi trilioni 13.17** ni kwa ajili ya matumizi ya Kawaida na **Shilingi trilioni 1.77** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Jedwali Na. 4: Maombi ya Fedha kwa Wizara ya Fedha na Mipango Mafungu yaliyochini yake pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2022/23

### 4.2. Maombi ya Fedha ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2022/23

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2022/23, Wizara ya Fedha na Mipango inaomba kuidhinishiwa matumizi ya jumla ya **Shilingi trilioni 15,011,348,698,828** kwa mafungu yote nane (8) pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Kati ya kiasi hicho, **shilingi bilioni trilioni 12,300,089,361,000, Shilingi bilioni 940,092,236.828** ni kwa ajili ya matumizi ya Kawaida na **Shilingi bilioni 1,782,094,036** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

**Jedwali Na. 4: Maombi ya Fedha kwa Wizara ya Fedha na Mipango Mafungu yaliyochini yake pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2022/23 "000"**

| FUNGU | MATUMIZI MENGINEYO | MISHAHARA | MIRADI YA MAENDELEO | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| 01 | 9,093,984,694 | - | - | 9,093,984,694 |
| 07 | 37,229,786 | 5,142,226 | 1,590,000 | 43,962,012 |
| 10 | 2,048,142 | 934,162.828 | - | 2,982,304,828 |
| 13 | 2,915,586 | - | 470,000 | 3,385,586 |
| 21 | 809,482,970 | 855,178,117 | 1,741,003,099 | 3,405,664,186 |
| 22 | 2,214,380 | 9,452,132 | - | 2,223,831,932 |
| 23 | 39,551,734 | 6,361,101 | 2,844,792 | 48,757,627 |
| 50 | 40,658 | 48,267,019 | 25,259,210 | 114,184,139 |
| **JUMLA** | **12,240,250,622** | **925,334,757,828** | **1,771,167,101** | **14,936,752,481** |
| 45 | 59,838,739 | 14,757,479 | 10,926,935 | 74,596,218 |
| **JUMLA KUU** | **12,300,089,361** | **940,092,236.828** | **1,782,094,036** | **15,011,348,698,828** |

*Chanzo: Randama za Mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya CAG.*

## 5.0. MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI FUNGU 45 KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi katika kutekeleza vipaumbele vyake imepanga kutumia jumla ya **Shilingi 86,423,153,000** katika mwaka wa fedha 2022/23. Kiasi hicho kinajumuisha **Shilingi milioni 900** fedha za Maduhuli kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali na **Shilingi bilioni 85,523,153,000** fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo. Fedha za Matumizi ya Kawaida zinazoombwa ni **Shilingi bilioni 74,596,218,000** ambazo zinajumuisha **Shilingi 14,757,479,000** fedha za Mishahara ya Watumishi na **Shilingi bilioni 59,838,739,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Kwa upande wa fedha za Miradi ya Maendeleo kiasi kinachoombwa ni **shilingi 10,926,935,000** kati ya fedha hizo Shilingi **bilioni 7,828,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 3,098,935,000** fedha za nje.

**Jedwali Na. 3: Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Fungu 45 kwa mwaka 2022/23**

| Maelezo | Bajeti iliyoidhinishwa 2021/22 (A) | Mkadirio Mwaka 2022/23 (B) | Tofauti (B-A) | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| **MATUMIZI YA KAWAIDA** | | | | |
| Mishahara | 13,346,294,000 | 14,757,479,000 | 1,411,185,000 | 10.57 |
| Matumizi Mengineyo | 54,838,739,000 | 59,838,739,000 | 5,000,000,000 | 9.12 |
| **Jumla Matumizi ya Kawaida** | **68,185,033,000** | **74,596,218,000** | **6,411,185,000** | **9.40** |
| **1. MATUMIZI YA MAENDELEO** | | | | |
| 2.1 Fedha za ndani | 9,200,000,000 | 7,828,000,000 | (1,372,000,000) | -14.91 |
| 2.2 Fedha za nje | 2,714,902,000 | 3,098,935,000 | 384,033,000 | 14.15 |
| **Jumla Matumizi ya Maendeleo** | **11,914,902,000** | **10,926,935,000** | (987,967,000) | **-8.29** |
| **JUMLA FUNGU 45** | **80,099,935,000** | **86,423,153,000** | **6,323,218,000** | **7.89** |

*Chanzo: Randama ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi*

## 5.1. Maamuzi baada ya Mashauriano kuhusu Bajeti ya Fungu 45

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bajeti ilikamilisha majadiliano na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango na kubaini masuala yafuatayo: -

i. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iliomba nyongeza ya Bajeti ya **Shilingi bilioni 10.8** ili kukidhi mahitaji ya kaguzi. Kutokana na ukomo wa Bajeti Serikali ilikubali kuongeze fungu hilo **Shilingi bilioni 5** tu.

ii. **Shilingi bilioni 5.8** ambazo hazikuongezwa kulingana na maombi zilihusu ujengaji wa mifumo ya ukaguzi na ununuzi wa magari kwa ajili ya ukaguzi wa ufanisi;

iii. Utolewaji wa Fedha za matumizi mengineyo kwa mwaka wa Fedha 2020/21 haukufikia **asilima 100** na badala yake ilikuwa ni **asilimia 80.4** tu. Hivyo ni wazi kwamba ukaguzi haukufanyika kikamilifu.

iv. Fedha za maendeleo zilizotolewa kwa mwaka wa Fedha 2021/22 hadi mwezi Aprili ni **asilimia 66.6** ya Bajeti.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kubaini masuala hayo Kamati ilielekeza fungu hilo liongezewe jumla ya **Shilingi bilioni 3.9** kwa ajili ya matumizi yafuatayo:-

i. Kiasi cha **Shilingi bilioni 2.5** ili zikajenge na kuimarisha mifumo ya ukaguzi na usimamizi; na

ii. **Shilingi bilioni 1.4** ili zikanunue magari kwa ajili ya shughuli za ukaguzi mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kusisitiza ni vyema fedha hizo ziongezwe kwa Fungu hili hasa ukizingatia umuhimu wa ukaguzi na kuongezeka kwa mawanda ya ukaguzi. Hoja hii itakuwa ni moja ya hoja ambazo kamati ya Bajeti itashauriana na Serikali wakati wa majadiliano kwa mujibu wa kanuni ya 124(1) ili kuhakikisha jambo hili linapatiwa muafaka.

## 6.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya Kamati kupitia utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/22 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mafungu husika kwa mwaka wa fedha 2022/23. Kamati inapenda kutoa maoni na Mapendekezo ya ujumla kama ifuatavyo:-

### 6.1. Kuanzishwa kwa Fungu Jipya Namba 001 Deni la Serikali

**Mheshimiwa Spika,** Kwa niaba ya kamati ya kudumu ya Bunge ya Bajeti naomba kuwasilisha pongezi za dhati kwa Serikali kwa kukubali kuazisha Fungu jipya litakalokuwa linahusika na ulipaji wa Deni la Serikali tu. Hatua hii itaondoa mkanganyiko uliokuwepo wa kujumlisha madeni ya Serikali na huduma za mfuko wa Serikali.

### 6.2. Utekelezaji wa Miradi kwa njia ya Ubia baina ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma

**Mheshimiwa Spika,** Kama kuna njia nzuri na rahisi ya kujenga miundombinu ya mawasiliano, huduma, usafiri na usafirishaji ni kwa kutumia njia ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Pamoja na uwepo wa Sheria tangu mwaka 2010 njia hii haijaweza kulinufaisha Taifa hili kwa zaidi ya miaka 12 hadi hivi sasa. Mara kadhaa kamati imekuwa ikishauri Serikali kwanza kwa kufanya mabadiliko kwenye Sheria ya Ubia ili kupunguza kiwango cha mtaji kutoka dola za marekani **milioni 20** hadi walau kati ya dola za marekani **milioni 2** hadi **milioni 5** kwa Watanzania na kwa wageni kati ya dola **milioni 5** hadi **milioni 10.** Hatua hii si tu itavutia wawekezaji kutoka nje bali watanzania

wataweza kushiriki kwenye ujenzi na utoaji wa huduma kwa mfumo wa Ubia.

### 6.3. Utendaji wa Kazi wa Kikosi kazi cha Mabadiliko ya Kodi *“Task Force on Tax Reform”*

**Mheshimiwa Spika,** Kikosi kazi cha Mabadiliko ya Kodi kimeanzishwa kwa mujibu wa kanuni ya 9 ya Kanuni za Sheria ya Bajeti na majukumu yake yamebainishwa katika kanuni ya 10. Kazi kubwa ya kikosi kazi hicho ni kupokea maoni na mapendekezo yanayohusu mabadiliko ama ya sheria za kodi au utaratibu wa kukusanya kodi. Changamoto kubwa ya Kikosi kazi hicho ni kutokutoa mrejesho kwa wadau mbalimbali wanaofika mbele yake ili kuwajulisha ni kwanini mapendekezo yao hayajakubaliwa. Hali hii husababisha masuala yanayowasilishwa katika kikosi kazi kujirudia kila mwaka na hayafanyiwi kazi. Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu wa kutoa mrejesho kwa wadau waliofika mbele yake ili hoja zinazowasilishwa zisijirudie mara kwa mara bila majibu. Aidha, kamati inapendekeza kuangalia muundo wa wajumbe wa kikosi kazi hicho na itolewe fursa ya kualika wataalamu wengine pale inapobidi.

### 6.4. Kutofautisha majukumu ya Idara za Serikali kati ya ukusanyaji wa mapato na utoaji wa Huduma

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bajeti inatambua umuhimu wa maduhuli katika mapato ya Serikali. Hata hivyo, maduhuli kwa baadhi ya maeneo yanaondoa hamasa ya kutoa huduma na badala yake Wizara, Idara, au Mamlaka za Serikali hasa zile ambazo hazifanyi Biashara zinaanzisha au kutoza viwango vikubwa vya ada na tozo ili kukusanya maduhuli na kusahau kwamba jukumu lao la kwanza ni kutoa huduma. Mfano, Taasisi

yoyote inapotaka kupata Taarifa za mtu kwa matumizi ya rasmi kutoka NIDA zinatozwa shilingi 500 kwa kila taarifa anayoitaka muhusika. Hivyo ni wazi kwamba kazi inayofanywa na NIDA ya kusajili watanzania wote ili watambulike imegeuka kuwa biashara na si huduma tena.

### 6.5. Utekelezaji wa Blue Print kwa masuala ya kikodi

**Mheshimiwa Spika,** Moja ya changamoto kubwa iliyobainishwa na wafanyabiashara katika Mpango wa Uboreshaji wa Mazingira ya Biashara (Blueprint) ni wingi wa mamlaka za Udhibiti na Usimamizi *"Multiplicity of Regulatory Authoritie"* pamoja Mfumo wa Ulipaji wa Kodi, ada na tozo. Kamati imekuwa ikishauri ni kwanini Serikali isiangalie uwezekano wa kuanzisha Mamlaka moja ya udhibiti katika mamlaka hiyo kuwe na Idara mbalimbali kama vile za Usalama mahala pa kazi, viwango na ubora, uzito na nyinginezo. Aidha, kama ni lazima ziwepo basi mfumo wa malipo ya ada na tozo zao uhuishwe. Mfano badala ya mfanyabiashara mmoja kulipa TBS, OSHA, Wakala wa Vipimo kupitia hati za madai tofauti tofauti aweze kufanya hivyo kupitia dirisha moja. Kwakuwa hizi zote ni Taasisi za Serikali basi mgao ufanyike Serikalini. Hatua hii haiathiri mapato ya Serikali lakini inaleta ufanisi katika ukusanyaji wa fedha za Serikali.

### 6.6. Kuangalia uwezekano wa kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Manunuzi ya Umma

**Mheshimiwa Spika,** kuna haja ya kuangalia uwezekano wa kupitia upya sheria ya manunuzi ya umma ili iendane na wakati ili kutanzua changamoto mbalimbali ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wake, baadhi ya changamoto ni:-

i. Matumizi ya sheria hiyo kwa mashirika na Taasisi za Umma ambazo zinajiendesha kibiashara imekuwa na

changamoto kubwa. Mfano Shirika kama TTCL haliwezi kununua minara ambayo imetumika lakini bado iko kwenye hali nzuri kwa sababu sheria inahitaji wanunue minara mipya wakati huo huo shirika halina fedha za kutosha kununua minara mipya;

ii. Inachelewesha mchakato wa manunuzi katika mashirika ya umma yanayojindesha kibiashara ambayo maamuzi ya haraka yanatakiwa kufanyika ili biashara iendelee;

iii. Kipengele cha "*lowest evaluated bidder"* au mzabuni aliomba kwa bei ya chini kuliko wote kimekuwa kinatoa mwanya kwa wakandarasi kuungana na kuamua bei ya chini iwe ipi; na

iv. Sheria hii haitoi tofauti ya ununuzi wa vifaa muhimu kama vile dawa na vifaa tiba na ununuzi wa mabati au matofali

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kubadilisha sheria hiyo ili iendane na mahitaji ya sasa.

## 7.0. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge hili la Bajeti. Aidha, nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wote wa kuchambua utekelezaji wa Bajeti na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/22. Vilevile nimshukuru Katibu Mkuu Ndugu Emmanuel Tutuba, Manaibu Katibu Wakuu pamoja na Wataalam wote wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao. Kamati inatambua mchango wa Wakuu wa Taasisi na Idara zote zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango katika kujadili kuchambua na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee kabisa napenda kumshukuru Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Ndg. Charles Kichere kwa ushirikiano wake na ufafanuzi alioutoa kwa Kamati katika kipindi chote cha kujadili utekelezaji wa majukumu ya Ofisi yake kwa mwaka 2021/22 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/23.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho si kwa umuhimu naomba kuwapongeza wajumbe wa Kamati kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao walionipatia wakati wote wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Wizara hii na hatimaye kukamilika kwa Taarifa hii. Naomba kuwatambua wajumbe hao kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Daniel Baran Sillo, Mb | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Omari Mohamed Kigua, Mb | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Ali Hassan King, Mb | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Issa Jumanne Mtemvu, Mb | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Oran Manase Njeza, Mb | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Joseph George Kakunda, Mb | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Shally Josepha, Raymond, Mb | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Esther Nicholas Matiko, Mb | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Jonas William Mbunda, Mb | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Juma Hamad Omar, Mb | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Tarimba Gulam Abbas, Mb | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Amina Idd Mabrouk, Mb | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Riziki Said Lulida, Mb | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Halima James Mdee, Mb | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Zaytun Seif Swai, Mb | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Dkt. Charles Stephen Kimei, Mb | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Mariam Nassoro Kisangi, Mb | Mjumbe |
| 23. | Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa kuiwezesha Kamati katika kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Kamati inatambua na kuenzi mchango wa Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndg. Michael Kadebe kwa kuipatia ushauri wa kitaalam Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango yanayojumisha Mafungu nane (8) yaliyochini yake pamoja na Fungu 45 la Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2022/23 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.



Daniel Baran Sillo,
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**
7 Juni, 2022